# HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

**HOTUBA YA MSTAHIKI MEYA WA MANISPAA YA UBUNGO ALIYOISOMA KWENYE KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KUPITISHA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO KWA MWAKA 2018/2019 – 2019/2020**


IMETAYARISHWA NA:

HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO,
S.L.P. 55068,
DAR ES SALAAM
SIMU: 0222926341
FAX: 0222926342


**FEBRUARI, 2018**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO KWA MWAKA 2018/2019 – 2019/2020**

**Waheshimiwa Wajumbe wa**

**Baraza la Halmashauri ya Manispaa Ubungo**,

**Watendaji, Wana Habari,**

**Mabibi na Mabwana**

Msingi wa kuandaa bajeti hii unatokana na miongozo inayotolewa na Serikali Kuu mara kwa mara pamoja na maagizo ya viongozi wetu ambao wamekuwa wakiyatoa kwa lengo la kufanikisha kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020 yenye lengo la kuleta maendeleo kwa wananchi na inaenda sambamba na Mpango wa maendeleo wa miaka mitano. Mpango huu umejikita katika kujenga uchumi ulioimara, kuboresha na kudumisha huduma za jamii na kuzingatia msingi wa utawala bora na uwajibikaji. Mpango huu pia umezingatia Dira ya Taifa ya 2025 ambayo imeweka mkakati wa kuleta maendeleo endelevu kwa Watanzania wote, Malengo ya millenia yanayolenga kupunguza Umaskini, kuboresha mazingira na kuleta usawa wa kijinsia katika kuleta maendeleo.

***Waheshimiwa Wajumbe***, Kabla ya kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2018/2019 naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine kutayarisha bajeti hii, ambayo maandalizi yake yamehusisha wadau wengi. Napenda kuwashukuru wakazi wa Ubungo kwa pamoja walioshiriki zoezi la kuibua miradi katika ngazi ya Mitaa na Kata inayolenga kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii ambayo ndiyo tumeyafanyia kazi katika kuandaa bajeti hii. Nachukua fursa hii pia kuwashukuru Wajumbe wa Baraza la wafanyakazi, Wajumbe wote wa Kamati za kudumu ambao ni Kamati ya Fedha na Uongozi, Kamati Huduma za Uchumi, Afya na Elimu, Wajumbe wa Kamati ya Mipangomiji na Mazingira pia kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuchambua makisio yote ya Mapato na Matumizi pamoja na miradi ya Maendeleo. Ushauri wa wajumbe wa kamati umesaidia sana kuboresha bajeti ninayoiwasilisha leo. Maagizo ya ushauri wa kamati hizi zote ikiwemo na Baraza hili la leo vitajumuishwa kwenye hatua ya mwisho ya bajeti .

***Waheshimiwa Wajumbe,***

**MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2016/2017 NA MWAKA 2017/2018**

Kabla ya kuwasilisha bajeti ya mwaka 2018/2019 ni vyema tukapata fursa ya kujua mafanikio ambayo yamepatikana katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2016/2017 na 2017/2018, tunayoendelea nayo kwa sasa.

Tathmini inaonyesha kuwa katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2016/2017 na 2017/2018 Halmashauri metoa huduma kwa wananchi wake kwa ufanisi mkubwa pamoja na uchanga wa Halmashauri katika maeneo ya Elimu ya Msingi na Sekondari, Utoaji wa huduma za Afya, Uimarishaji wa miundombinu ya barabara, Uwajibikaji na Utawala Bora. Aidha Halmashauri imeimarisha upatikanaji wa nyenzo za kufanyia kazi kwa watumishi wake hali iliyoimarisha usimamizi wa kazi katika maeneo ya Miradi na utoaji wa huduma.

***Waheshimiwa Wajumbe***, katika bajeti ya mwaka 2016/2017 ilikadiria kukusanya/kupokea fedha kiasi cha Sh. **111.8 billioni** kutoka serikali kuu na mapato ya ndani ya Halmashauri. Hadi Juni 2017 fedha zilizopokelewa ni Tsh.9 Billioni na zilizotumika ni Tsh.6.9 Billioni sawa na asimia 77. Halmashauri ililenga kukusanya mapato ya ndani kiasi cha **Tshs.26 billioni** na kufanikiwa kukusanya **Tsh. 6.6 billioni.** Makusanyo ya ndani yako chini kwa kuwa Halmashauri ilianza rasmi mwezi Oktoba na kuanza kukusanya mapato mwezi Novemba na chanzo cha kodi ya majengo kukusanywa moja kwa moja na TRA.

Aidha fedha za mapato ya nje (ruzuku) zilizokadiriwa kupokelewa **ni Tsh.85 billioni** na kiasi kilichopokelewa ni **Tsh. 5.8 billioni** ambazo ni fedha za miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Fedha za mishahara zilipokelewa Halmashauri mama (Kinondoni).

***Waheshimiwa Wajumbe***, katika bajeti ya mwaka 2017/2018

Katika mwaka wa fedha **2017/20118** Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo inatarajia kukusanya/kupokea fedha kiasi cha **Tsh. 97.5 billioni** Kati ya fedha hizo **Tsh. 11.3 billioni** ni Ruzuku ya miradi ya maendeleo kutoka Serikali Kuu, **Tsh. 62.8 billioni** ni Ruzuku ya matumizi ya kawaida na mishahara kutoka Serikali Kuu, **Tsh. 22.5billioni** ni fedha za makusanyo ya ndani ya Halmashauri na **Tsh. 750 millioni ni** za michango ya nguvu za wananchi. Hadi Desemba, 2017 jumla ya Tsh.**20.6** zimepokelewa sawa na asilimia 21 ya makisio ya bajeti na kiasi cha Tsh **4.8 billioni** zimetumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

Aidha katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Halmashauri ililenga kukusanya mapato ya ndani kiasi cha **Tshs. 22.5 billioni** , Hadi Desemba 2018 **Tshs. 7.1billioni** kimekusanywa sawa na **asilimia 32** ya lengo. Ili kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani hatua kadhaa zimechukuliwa ambazo ni pamoja na kutumia mfumo wa Kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, kufanya operesheni za ukusanyaji mapato mara kwa mara, kuimarisha timu za ukusanyaji na ufuatiliaji wa mapato kwa kila chanzo cha mapato zilizochini ya mameneja na kuimarisha takwimu za walipa kodi.

***Waheshimiwa Wajumbe,***

**UJENZI NA MIUNDO MBINU**

Katika kipindi cha mwaka 2016/2017 Halmashauri iliweka mkakati wa kuchonga barabara zake, kujenga mifereji na madaraja ili kuimarisha miundombinu ya barabara. Hadi mwezi Juni, 2017 maeneo muhimu yaliyotekelezwa ni pamoja na:-

- Ujenzi wa Daraja la Mbezi Msumi kwa Londa.
- Ukarabati mdogo wa barabara za kata zote 14.
- ujenzi wa vivuko vya waenda kwa miguu Kilimahewa - Makurumla na Upendo-Kimara.
- Matengenezo ya barabara ya Makoka pattaya Kata ya Makuburi, Manzese Midizini.
- Ujenzi wa mfereji wa maji ya mvua barabara ya Watani mpaka Shule ya msingi Mianzini, Kusawazisha na kutengeneza mifereji katika Shule ya Msingi Saranga yamekamilika.
- Ukarabati wa barabara ya Kimara Baruti - Uwanjani na Kusawazisha na kutengeneza mifereji katika Shule ya Msingi King'ongo unaendelea.

***Waheshimiwa Wajumbe,***

**SEKTA YA ELIMU**

Halmashauri kwa mwaka 2016/2017 iliweka lengo la kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya Sekondari kufikia asilimia **100%** kwa mwaka 2017. Usajili wa wanafunzi wa kidato cha kwanza umeongezeka kutoka asilimia 85% mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 100% mwaka 2007. Aidha Halmashauri imefanikiwa kujenga shule mpya ya Kata-Kimara ambayo tayari imeshaanza kuchukua wanafunzi. Jumla ya wanafunzi 198 wa kidato cha kwanza wameandikishwa katika shule hiyo.

Halmashauri kwa mwaka 2016/2017 iliweka lengo la kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa darasa la kwanza. Lengo la uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza kwa mwaka 2017 lilikuwa ni kuandikisha wanafunzi 12,585.00 na wanafunzi walioandikishwa ni 11,638.00 sawa na asilimia 92 ya lengo.

Mikakati iliyopo ni kuendelea kuimarisha miundombinu katika sekta ya Elimu ikiwemo, kufanya ukarabati wa majengo chakavu, ujenzi wa madarasa, kununua madawati pamoja na ujenzi wa vyoo na nyumba za walimu. Kutokana na sera ya Serikali ya kutoa elimu bila malipo kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaoandikishwa.

Katika kuboresha sekta ya elimu Msingi na kukabili ongezeko kubwa la wanafunzi walioandikishwa, halmashauri imefanikiwa kujenga na kukarabati madarasa 68, ujenzi wa matundu 60 ya vyoo na ukamilishaji wa nyumba 2 za walimu katika shule za msingi umefanyika.

***Waheshimiwa Wajumbe***,

**HUDUMA ZA AFYA**

Halmashauri katika kipindi cha mwaka 2016/2017-2017/2018 Halmashauri imeendelea kupanua na kuboresha huduma za Afya kwa kuboresha upatikanaji wa madawa na vifaa tiba katika vituo vya afya, kuboresha miundombinu ya afya kwa kujenga mfumo wa maji taka hospitali ya Sinza, ujenzi wa choo cha wagonjwa na kichomea taka zahanati ya Mburahati, Umaliziaji wa zahanati ya Malambamawili na Ujenzi wa uzio zahanati ya Mabibo. Aidha Halmashauri imejipanga kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto kwa kujenga jengo la wazazi Kituo cha Afya Kimara na Makurumla na kujenga jengo la kuhifadhia chanzo zahanati ya Mabibo na kununua jenereta kubwa Hospitali ya Sinza ili kukabiliana na tatizo la kukatika kwa umeme.

Aidha, Halmashauri imefanikiwa kuwatambua na kuwafiikia wazee 7,299 kati ya hao wazee 3,600 wameshapata vitambulisho vya msamaha wa matibabu kwa ajili ya kuwawezesha kupata kadi ya bima ya afya (TIKA). Zoezi hili linaendelea.

***Waheshimiwa Wajumbe,***

**HUDUMA YA MAJI:**

Katika kipindi cha mwaka 2016/2017 na 2017/2018 Halmashauri iliweka lengo la kupanua na kuboresha miradi ya usambazaji maji katika maeneo mbalimbali. Katika Manispaa ya Ubungo Jumla ya wakazi 670,377 ambao walikuwa asilimia **65** ya walengwa wote wanapata huduma ya maji. Hadi Desemba, 2017 Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo inaendelea kutekeleza miradi kadhaa ya maji ili kuongeza upatikanaji wa maji. Utekelezaji wa Mipango ya miradi ya maji inakwenda sambamba na uanzishwaji kwa miradi mipya ya maji, ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji.

- Ujenzi wa mradi wa usambazaji maji katika Mtaa wa Makabe uko hatua ya manunuzi.
- Mradi wa usambazaji maji Gogoni Kibamba unaendelea
- Ukarabati wa mradi wa usambazaji maji katika Mtaa wa Mpiji Magohe unaendelea
- Upanuzi wa mradi wa usambazaji maji katika Mtaa wa Kibwegere umekamilika na unafanya kazi
- Upanuzi wa mradi wa usambazaji maji katika Mtaa wa King'azi A umekamilika na unafanya kazi
- Ukarabati wa mradi wa usambazaji maji katika Mtaa wa Kiluvya unatarajia kuanza robo ya tatu.

***Waheshimiwa Wajumbe,***

**HUDUMA ZA KIUTAWALA**

Katika kipindi cha mwaka 2017/2018 Halmashauri iliweka lengo la kuboresha mazingira kufanyia kazi kwa watumishi na Waheshimiwa Madiwani kwa kufanya yafuatayo;

- Kujenga jengo la Ofisi za Manispaa ya Ubungo. Hadi sasa mradi huu uko kwenye hatua ya upembuzi yakinifu wa eneo la ujenzi. Ujenzi utaanza pindi taratibu hizi zikikamilika.
- Kununua vitendea kazi mbalimbali kama kompyuta, magari kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato hasa ukizingatia Halmashauri yetu ni mpya. Hadi sasa magari aina ya 'double cabin' yamenunuliwa
- Genereta kubwa limenunuliwa kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kijamii muda wote pindi umeme wa TANESCO unapokatika
- Upatikanaji wa stahiki za watumishi na Waheshimiwa Madiwani umeendelea kuboreshwa kutokana na upatikanaji wa fedha.

***Waheshimiwa Wajumbe,***

Katika utekelezaj wa bajeti na mpango wa maendeleo wa mwaka 2016/2017 na 2017/2018 zilijitokeza changamoto kadhaa, hususani ufinyu wa rasilimali kulinganisha na ukubwa wa mahitaji halisi ya utoaji huduma, Kuchelewa kwa fedha za baadhi ya miradi kutoka Serikali na upungufu wa Wahandisi kwa ajili ya kuaandaa BOQ za miradi na hivyo kupelekea taratibu za manunuzi kuchelewa na miradi ya maendeleo kuchelewa kuanza kutekelezwa kwa mujibu wa mpango kazi wa

bajeti. Hata hivyo, napenda kuchukua fursa hiyo kuwapongeza Waheshimiwa Madiwani ambao kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kata zao wametoa michango yao kusaidiana na Halmashauri katika utoji wa huduma kwa wananchi.
Tunaomba jitihada hizo ziendelee katika utekelezaji wa bajeti ya 2018/2019 itakayopitishwa leo.

***Waheshimiwa Wajumbe,***

**MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA 2018/2019**

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa mwaka 2018/2019 imekadiria kukusanya na kupokea jumla ya **Tshs. 98,238,193,600.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikali Kuu, mapato yake yenyewe, Wahisani na mchango wa wananchi. Kati ya fedha hizo Mapato ya Manispaa (own source) yanatarajiwa kuwa **Tsh. 25,691,278,000.00,** Ruzuku kutoka Serikali Kuu na Wafadhili ni **Tshs. 71,796,915,600.00** na wananchi wanatarajiwa kuchangia **Tshs. 750,000,000.00.**

***Waheshimiwa Wajumbe,***

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa mwaka 2018/2019 imekadiria kutumia fedha kiasi cha **Tsh. 98,238,193,600.00.** Kati ya fedha hizo **Tsh. 76,607,163,700.00** ni matumizi ya kawaida na mishahara ambayo ni sawa na asilimia **78** ya bajeti yote na **Tsh. 21,631,029,900.00** ni fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia **22** ya bajeti yote.

***Waheshimiwa Wajumbe,***

Kwa mwaka 2018/2019 Halmashauri itatumia jumla ya **Tshs. 71,796,915,600.00** ikiwa ni ruzuku, sawa na asilimia **100** kutekeleza vipaumbele vya maendeleo na maeneo ya utoaji wa huduma.

Kati ya fedha hizi mishahara ni **Tsh. 61,923,432,600.00** ikiwa ni mishahara, matumizi ya kawaida ni **Tsh.1,593,213,500.00** na miradi ya maendeleo ni **Tsh. 8,280,269,500.00**. Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha mfuko wa afya (HSBF), Fedha za ruzuku ya maendeleo na kujenga uwezo (LGCDG), fedha za Programu ya maji vijijini (RWSSP), Fedha za mfuko wa Jimbo (CDF) na Programu ya Elimu bure msingi na Sekondari,

***Waheshimiwa Wajumbe***,

Halmashauri kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 itatumia **Tshs. 25,691,278,000.00** kutoka katika mapato ya ndani kwa matumizi mengineyo, mishahara, miradi ya maendeleo na uchangiaji (Cost sharing). Aidha **Tshs. 12,600,760,400.00** zitatumika kutekeleza miradi ya maendeleo sawa na asilimia 49% na **Tshs. 8,307,173,600.00** sawa na asilimia 32% zitatumika katika maeneo ya uendeshaji wa shughuli za ofisi na **Tshs.191,544,000.00** sawa na asilimia 1% zitatumika katika kulipa mishahara ya watumishi na **Tsh. 4,591,800,000.00** ni uchangiaji (cost sharing).

***Waheshimiwa Wajumbe,***

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imekidhi kigezo cha kutenga asilimia **60** ya fedha za mapato yake ya ndani katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Jumla ya **Tsh. 12,600,760,400.00** sawa na asilimia **60** ya fedha za mapato ya ndani imetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na **Tsh.8,498,717,600** sawa na asilimia **40** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara.

***Waheshimiwa Wajumbe,***

Katika kufanikisha malengo hayo bajeti ya mwaka 2018/2019 imeweka vipaumbele katika maeneo yafuatayo:

i. kuimarisha utawala bora na utoaji huduma kwa jamii kwa kujenga jengo la ofisi ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ambapo kiasi cha **Tsh 3,000,000,000/-** kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo hilo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

ii. Kuongeza na kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kutumia mfumo wa kielektroniki kutoka **Tsh. 22.5 Bilioni** kwa sasa hadi **Tsh. 25.7 Bilioni** kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

iii. Kuboresha utoaji huduma kwa wananchi kwa kutekeleza miradi ya maendeleo hivyo Kiasi cha **Tsh. 21,631,029,900/=** kimetengwa kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

iv. Kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa kununua madawa na vifaa tiba, Kujenga na kuboresha miundo mbinu ya afya katika hospitali ya Sinza, Vituo vya Afya na zahanati. Jumla ya **Tsh. 8.2 Bilioni** zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

v. Kusimamia na kutoa mafunzo, ziara, stahiki na posho za Waheshimiwa Madiwani pamoja na Wajumbe na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ambapo Kiasi cha **Tsh. 235,923,028/=** kimetengwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

vi. Kuboresha miundombinu ya barabara kwa kujenga Madaraja/Makalvati, barabara kwa kiwango cha lami, kufanya matengenezo ya kawaida ya barabara, muda maalum, maeneo korofi, njia za waenda kwa miguu, Ujenzi wa vivuko vya waenda kwa miguu na Mifereji katika barabara za Manispaa. Jumla ya **Tsh. 1.4 Bilioni** zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

vii. Kukuza uchumi na kujenga miundombinu katika sekta za afya, elimu, maji na masoko kwa kutwaa ardhi, kulipa fidia maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya uwekezaji hivyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Kitengo cha Uthamini kimetengewa **Tsh.1,200,000,000/=** kwa ajili ya kutekeleza shughuli hizo.

viii. Kutoa mikopo kwa wanawake na vijana kwa mujibu wa miongozo ya Kitaifa ili kuchochea maendeleo na ukuaji wa kipato kwa wananchi ambapo kiasi cha **Tsh 1,144,428,098/=** kimetengwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

ix. Kuimarisha na kujenga miundombinu ya michezo kama viwanja vya michezo pamoja na kijiji cha michezo ambapo kiasi cha **Tsh. 100,000,000/=** kimetengwa. Halmashauri pia imetenga **Tsh. 50,000,000/=** kuanzisha Mashindano ya **'*Meya cup*'**.

x. Kuongeza kiwango cha uzoaji taka ngumu Manispaa kwa kununua magari, mitambo na vifaa vya usafi wa mazingira

jumla ya **Tsh. 1,200,000,000/=** kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

xi. Kujenga na kuboresha majengo ya utawala na miundombinu, ofisi za walimu Shule za Msingi na Sekondari kiasi cha **Tsh. 300,000,000/=** kimetengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019

xii. Kuboresha utoaji huduma za ushauri na ugani kwa wakulima na wafugaji hivyo kiasi cha **Tsh.120,227,200/=** kimetengwa kwa ajili ya marekebisho ya baadhi ya miundombinu na ujenzi banda la maonyesho Nane nane Tungi-Mororogoro.

xiii. Kuboresha huduma ya usambazaji maji safi na salama kwa wananchi hivyo Kiasi cha **Tsh.1,303,129,500/=** kimetengwa kwa ajili ya Miradi ya maji kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

xiv. Kuboresha huduma za afya kwa Wazee kwa kuhakikisha kuwa kila mzee aliyetambuliwa anapata Kadi ya Bima ya afya kwa ajili ya matibabu hivyo kiasi cha **Tsh. 60,000,000/=** kimetengwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

xv. Kupanua wigo wa kutolea huduma za afya kwa jamii kwa kujenga Hospitali ya Wilaya ya Ubungo hivyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 **Tsh. 100,000,000/=** zimetengwa kwa ajili ya mchakato wa Uthamini na kwa ajili ya kupata eneo la kujenga Hospitali hiyo.

xvi. Kufanya ujenzi wa machinjio ya Wilaya ya ubungo ikiwa ni mkakati wa kukuza mapato hivyo Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kiasi cha **Tsh.150,000,000/=** kimetengwa kwa jili ya ujenzi wa machinjio ya kuku ya kisasa Shekilango pamoja na

kufanya upembuzi yakinifu wa Machinjio ya kisasa ya Ng'ombe Luguruni.

xvii. Kuendelea kuboresha na kujenga masoko ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo. Kiasi cha Tsh. **450,000,000/=** kimetengwa katika bajeti ya mwaka 2018/2019

***Waheshimiwa Wajumbe,***

**HITIMISHO:**

Mpango na bajeti umejikita katika kutekeleza malengo ya maendeleo endelevu pamoja na Mpango wa Maendeleo wa miaka 5 (2016/2017 – 2020/2021) na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Ili kufikia malengo tuliyojiwekea hakuna budi kila mwananchi, Waheshimiwa Madiwani na Watendaji kushiriki kikamilifu kwa kutumia fursa zilizopo katika kuleta maendeleo ili kuondokana na umaskini.

***Waheshimiwa Wajumbe***,

Baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha Bajeti ya mwaka 2018/2019 katika Kikao cha Baraza tukufu kama ilivyoainishwa kwenye kitabu cha Bajeti.

Naomba kuwasilisha.

**MSTAHIKI MEYA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO**